JINA LA MTAHINIWA..... JINA LA SHULE.....

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA KILIMANJARO

MTIHANI WA MHULA WA II – DARASA LA TATU

JIOGRAFIA

Muda: Saa 1:30
Novemba 2024

MAELEKEZO:

1. *Mtiahani huu unavipengele Ana B yenye jumla ya maswali manne.*
2. *Jibu maswali yote kwa kila kipengele.*
3. *Andika majibu yako katika sehemu iliyoachwa wazi.*
4. *Majibu yote yaandikwa kwa kutumia kalamu ya wino wa bluu au mweusi.*

SEHEMU A:

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika swali la i-viii kisha iandike katika nafasi iliyoachwa wazi;

i. Ni katika umbo gani la sura ya nchi kati ya yafuatayo linaweza kusabisha kutokea kwa aina mojawapo ya mvua _____
   (a) tambarare
   (b) bonde
   (c) mlima
   (d) besini

ii. Nilimwona John akiwa anavaa sweta na nguo nzito kwa sababu alikuwa anatetemeka. Je sehemu hiyo ilikuwa na hali gani ya hewa?____
   (a) Joto
   (b) Jua
   (c) Baridi
   (d) Mvua

iii. Kwa nini vilele vya baadhi ya milima kama vile mlima Kilimanjaro vimefunikwa na barafu? _____
   (a) kuna joto kali
   (b) kuna mvua nyingi
   (c) kuna baridi kali
   (d) kuna maji mengi

iv. Mlima Kilimanjaro una urefu gani? _____
   (a) meta 5985
   (b) meta 9855
   (c) meta 5895
   (d) meta 5859

v. Ni kifaa kipi kati ya vifuatavyo hakitatumika kufanyia usafi katika darasa lenye sakafu ya vumbi?
(a) ufagio wa kutoa tandabui (c) Ufagio
(b) Dekio (d) Ndoo ya taka

vi. Ili kuvuta hewa safi na salama tunatakiwa kuzuia vyanzo vyote vya uchafuzi wa hewa kama .....
(a) Kuogea maji ya viwandani
(b) Kunywesha mifugo kwenye vyanzo vya maji
(c) Moshi kutoka viwandani
(d) Kufulia nguo kwenye vyanzo vya maji

vii. Ni ipi kati ya hewa zifuatazo zinahusika Zaidi katika ongezeko la joto katika uso wa dunia?_____
(a) oksjeni
(b) vumbi
(c) kabondayoksaid
(d) hidrojeni

viii. Zifuatazo ni umuhimu wa miti isipokuwa
(a) Kutupatia kivuli
(b) Kusababisha mvua
(c) Kutupatia dawa
(d) Kusababisha mafuriko

2. Oanisha maana kutoka kifungu A na maneno yaliyo katika kifungu B

KIFUNGU A	JIBU	KIFUNGU B
(i) Kitu gani ambcho matokeo yake ni muhimu kwa maisha ya binadamu		A. Miundombinu
(ii) Jumla ya vitu vyote vinavyomzunguka binadamu		B. Hali ya hewa
(iii) Inajumuisha maziwa,bahari,mito,chemchem na mabwawa		C. Majanga
(iv) Shughuli zote zinazofanywa na binadamu ili kujipatia kipato katika Maisha ya kila siku		D. Mazingira
(v) Inajumuiasha hospitali,reli,benki na barabara		E. Shughuli za binadamu
(vi) Mwenendo wa hali ya hewa inayoshuhudiwa katika eneo kwa muda mrefu mara nyingi zaidi ya miaka 30 huitwa		F. Vyanzo vya maji
		G. Shughuli za kisiasa
		H. Rasilimali


3. (a) Panga maumbo yafuatayo ya sura ya nchi kwa kuzingatia hali ya muinuko.Panga kuanzia umbo lenye muiniko mkubwa hadi lenye muinuko mdogo zaidi kwa kuyapa namba 1,2,3 na 4 kwenye visanduku vya majibu ulivyopewa

   i. Tambarare ( )
   ii. Mlima ( )
   iii. Kilima ( )
   iv. Uwanda wa juu ( )

   (b)Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuandika jibu sahihi kwa maswali yafuatayo

   i. Kwanini ni muhimu kuhifadhi mazingira?
   .....
   ii. Ni taasisi ipi ilianzishwa na serikali ya Tanzania kwa ajili ya kusimamia utunzaji wa mazingira? .....
   iii. Ni mahali panapofanyika shughuli za kiuchumi zinazohusisha uchakataji wa malighafi na kuzalisha bidhaa kwa kutumia mashine .....

4. Chunguza picha hapo chini kisha jibu maswali yanayofuata.



   (i) Eleza unachokiona katika picha hapo juu _____
   (ii) Je, unafikiri nini chanzo cha ulichokiona hapo juu? _____
   (iii) Nini athari ya janga lililotokea hapo juu ?_____
   (iv) Je, nini kifanyike ilikuzuia janga hilo hapo juu? _____